TANGAZO LA SERIKALI Na. 1031 La Tarehe 11/12/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA. 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA STENDI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi ya Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli, za Mwaka 2020.

Eneo la Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa itakavyotamkwa vinginevyo;-

*"Afisa Mwidhiniwa"* maana yake ni Afisa yeyote wa Halmshauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

*"Chombo cha Usafiri"* maana yake ni chombo cha moto ikijumuisha gari au pikipiki ya magurudumu mawili au matatu .

*"Halmshauri"* maana yake Halmshauri ya Wilaya ya Bumbuli.

*"Kituo cha basi"* maana yake ni kituo cha basi kilichoidhinishwa na Halmashauri ambapo mabasi yanatoa huduma ya kushusha na kupakia abiria.

*"Mkurugenzi*" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi

Sura 212

*"Ushuru wa stendi"* maana yake ni ushuru unaotozwa na Halmashauri kwa mtu yeyote anayeingiza chombo cha usafiri katika eneo la stendi.

*"Wakala"* maana yake ni Kampuni yoyote iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni na kukubaliwa na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri

Usimamizi wa stendi

4(1) Ni wajibu kila mmiliki wa magari ya abiria na mizigo yatokayo na yaendayo mikoani na maeneo yaliyo ndani na nje ya Mamlaka, kuingia katika eneo lilotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo.

(2) Isipokuwa kwa kibali maalum kutoka Halmashuri, mab kuanza safari zake katika stendi iliyotengwa katika stendi

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya matengenezo ya a ndani ya eneo la stendi.

Ushuru wa stendi

5(1) Halmashauri itatoza Ushuru wa vyombo vya usafiri vinavyoingia katika eneo la stendi ya mabasi kwa namna na kiasi kilichoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu wa kila mmiliki wa gari au chombo chochote cha usafiri kuhakikisha kwamba amelipia Ushuru wa Stendi kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(3) Vituo vya mabasi vitafunguliwa saa kumi na moja asubuhi na kufungwa saa nne usiku.

(4) Ushuru wa stendi utalipwa kwa siku au mwezi kadri Halmshauri itakavyoona inafaa.

(5) Ushuru wa stendi utalipwa kila gari linapotoka stendi kuanza au kuendelea na safari zake.

Usafi wa mazingira

6(1) Halmashauri itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba vituo vyote vinabaki katika hali ya usafi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazohusiana na mambo ya Afya na Mazingira.

(2) Kila mmiliki wa gari atahakikisha anaweka chombo cha taka ndani ya gari lake na kutunza uchafu huo ili kuweka hali ya kituo atakachoingia bila kufanya uchafuzi wa mazingira.

(3) Haitaruhusiwa kwa abiria au mtu yeyote yule kutupa taka ovyo, kumwaga maji ovyo au kutiririsha maji, kuosha gari au chombo chochote cha usafiri ndani ya stendi.

Makosa

8. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

a) atakataa kuingia katika eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo;
b) atajaribu au atakusanya Ushuru wa Stendi bila idhini ya Halmashauri;
c) atajaribu au atakusanya Ushuru wa Stendi kwa kiwango tofauti na kilichoidhinishwa na Sheria Ndogo hizi;
d) atashindwa kutoa stakabadhi halali ya malipo kwa Ushuru wa Stendi aliokusanya kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;
e) atashindwa kulipa Ushuru wa stendi
f) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kutolipa kulipa Ushuru;
g) ataegesha chombo cha usafiri katika eneo ambalo halijaainishwa na Halmshauri;
h) ataosha au utatengeneza chombo cha usafiri katika eneo la maegesho,

Adhabu

9. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote viwili kwa pamoja faini na kifungo.

Kufilililsh a makosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa Kufilililisha kosa kwa kumtoza faini mkosaji isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (1,000,000/=) kwa mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatanishwa katika Jedwali la Pili Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*( Limetungwa chini ya kifungu cha 5(2) )*

USHURU WA MAGARI YA ABIRIA NA MIZIGO

| Na. | Aina ya Gari | Kiasi cha Ushuru | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Mabasi makubwa | 5000 | Kwa siku |
| 2. | Mabasi ya Kati ( Coaster ) | 1500 | Kwa siku |
| 3. | Magari Madogo ( Hiace ) | 1000 | Kila linapoingia stendi |
| 4. | Taxi, Pick – Up, Kirikuu, Bajaji ikiegesha ndani ya kituo cha basi | 1000 | Kwa siku |
| 5. | Taxi, Pick – Up, Kirikuu, Bajaji ikiegesha nje ya kituo cha basi | 500 | Kwa siku |
| 6. | Pikipiki ikiegesha ndani ya kituo | 500 | Kwa siku |
| 7. | Pikipiki ikiegesha nje ya kituo | 300 | Kwa siku |
| 8. | Gari binafsi ikiegesha nje ya kituo | 300<br>600<br>1000 | - Kwa nusu saa<br>- Kwa saa<br>- Kwa siku |
| 9. | Taxi, pick-up, kirikuu, bajaji | 300 | Kila linapoingia ndani ya stendi kushusha abiria na kutoka. |
| 10 | Gari binafsi kuingia stendi | 1000 | Kwa siku |
| 11. | Pikipiki | 200 | Kila inapoingia ndani ya stendi kushusha abiria na kutoka. |

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 10)*

KUFILILISHA MAKOSA

Mimi………………………………………………wa S.L.P……………….................ninayeishi …………………………nakiri kuwa leo tarehe…………………nilikiuka kifungu cha………………cha Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi za Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli ya Mwaka 2020. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa kiasi cha ushuru ninachodaiwa pamoja na faini ilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa madaraka aliyopewa Mkurugenzi chini ya kifungu cha Sheria Ndogo hizi.

Sahihi………………………………………………………….

MBELE YANGU:

JINA……………………………………………………………

SAINI…………………………………………………………..

WADHIFA…………………………………………………

Nembo ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizo kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli uliofanyika mnamo tarehe 19/2/2020 na Nembo iliyogongwa mbele ya:-

GEORGE D. HAULE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bumbuli*

AMIRI A. SHEIZA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bumbuli*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Novemba, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.)
*WN-OR-TAMISEMI*